



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FB.111/192/01/38

30 Aprili, 2026

Kwa Taasisi Nunuzi Zote,

Yah: MWALIKO WA KUSHIRIKI KONGAMANO LA KUMI LA UNUNUZI WA UMMA LA MWAKA, 2026

Tafadhali rejeeni barua yangu yenye Kumb. Na. FB.111/192/01/17 ya tarehe 14 Aprili, 2026 ikiwa na somo tajwa hapo juu.

2. Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kukujulisha kuwa Kongamano la Kumi la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2026 (**10th Annual Procurement Governance Workshop, 2026**) ambalo awali lilipangwa kufanyika kuanzia tarehe **29 Juni hadi 1 Julai, 2026**, sasa linatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **29 hadi 31 Julai, 2026** katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), Jijini Arusha.
3. Kongamano la Ununuzi wa Umma ni jukwaa linalotoa fursa ya majadiliano, Mafunzo ya kitaaluma, kutafakari sera na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya ununuzi wa umma nchini. Kongamano hili litawaleta pamoja taasisi za umma, vyombo vya usimamizi na udhibiti, wataalamu wa ununuzi, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za kitaaluma (vyuo na watafiti), asasi za kiraia, pamoja na makundi maalum ili kujadili changamoto za utekelezaji wa shughuli za wa ununuzi wa umma na fursa zinazoibuka.
4. Kongamano la Ununuzi wa Umma la Mwaka 2026 litakuwa na dhima inayosema: **“Kutumia fursa ya Ununuzi wa Umma Kidijitali kufikia Uchumi Endelevu, Shirikishi na Shindani kuelekea Dira 2050.”**
5. Mamlaka inazialika taasisi nunuzi zote nchini kushiriki kongamano hili muhimu. Wanaopaswa kushiriki Kongamano hili ni Maafisa Masuuli, wajumbe wa bodi za zabuni, maafisa ununuzi, wanasheria, wakaguzi wa ndani, watumishi kutoka idara tumizi, wafanyabiashara, watafiti, wanafunzi, asasi za kiraia na wengineo.
6. Ili kuweza kushiriki katika Kongamano hili, washiriki wanatakiwa kujisajili katika Mfumo wa mafunzo wa PPRA kupitia anuani <https://tsms.gov.go.tz/> au

<https://tsms.ppra.go.tz/>. Ada ya ushiriki ni shilingi 600,000 kwa kila mshiriki. Mwisho wa kufanya usajili ni tarehe **30 Juni, 2026**.

7. Kwa taarifa au ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Bw. Fikiri Ngakonda, kupitia namba 0714 928 154 barua pepe: fikiri.ngakonda@ppra.go.tz au Bw. Emmanuel Simbeye, kupitia namba ya simu 0713 228 182 barua pepe: emmanuel.simbeye@ppra.go.tz.

8. Asanteni kwa ushirikiano wenu.


Dennis K. Simba
MKURUGENZI MKUU